# Sababu za Kuibuka, Kung'ara, na Kupotea kwa Wasanii katika Tasnia ya Muziki wa Bongo Fleva: Uchunguzi wa Kategoria Maalumu ya Nyimbo Hizo

*Issaya Lupogo*
*Chuo Kikuu Mzumbe*
*islupogo@Mzumbe.ac,tz*

## Ikisiri

Muziki wa Bongo Fleva (BF) umekua kwa kiasi kikubwa sana nchini Tanzania. Muziki huo sasa umekuwa biashara tofauti na miaka ya 2000 ambapo wasanii waliishia kuwa maarufu tu bila kupata kipato kikubwa kama miaka ya hivi karibuni (miaka ya 2015 hadi sasa). Jambo la kushangaza na ambalo limemakinikiwa katika makala haya ni kwamba wasanii wengi wa Bongo Fleva huibuka na kung'ara zaidi kwa muda fulani katika muziki lakini baadaye hupotea katika tasnia hii. Kwa hivyo, makala haya yanaangazia sababu za wasanii hao kuibuka, kung'ara, na kupotea. Matokeo ya makala haya yametokana na tajriba ya mwandishi kwa kuwa yeye ni mdau mkubwa wa masuala ya muziki. Mwandishi ni msanii[1] wa muziki wa BF kwa kiasi fulani na amekuwa akishiriki katika kipindi cha redio[2] ambacho pamoja na mambo mengine, huchambua habari za wasanii na kufanya nao mahojiano. Mwandishi pia amekuwa akifuatilia kwa karibu habari za wasanii na sanaa ya BF kupitia vyanzo mbalimbali vya habari. Wasanii waliomakinikiwa na kutumiwa kama sampuli ni wale wanaoimba muziki wa R & B, Zuku, Hip-hop, na Injili. Makala haya yamebaini kuwa mambo yafuatayo yanayowafanya wasanii kuibuka na kung'ara katika BF: Kuwa na kipaji kizuri cha kuimba, kujituma, na udhamini au menejimenti nzuri. Kwa upande mwingine makala pia yamebaini kuwa wasanii hao hupotea katika tasnia ya muziki kwa sababu mbalimbali: Sababu za kiuelewa (kuelewa mambo mbalimbali), sababu za kiutandawazi na usasa, sababu za kielimu (elimu ya darasani), sababu za kimenejimenti, migogoro baina ya wasanii, na kuingia mgogoro na Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA). Kutokana na matokeo hayo, mwandishi wa makala haya ameibua nadhariatete inayotawala mustakbali wa wasanii wa BF. Nadhariatete hii inaeleza

1 Hizi ni baadhi ya nyimbo za BF za mwandishi ambazo zipo YouTube
Wimbo wa 1 https://youtu.be/AHJjLuGRoCA
Wimbo wa 2 https://youtu.be/pBGkNmcPGHc
Wimbo wa 3 https://youtu.be/sKHqGW9t4hk
Wimbo wa 4 https://youtu.be/PV4afS2uhio

2 Mwandishi huwa anaalikwa kila Ijumaa katika kipindi cha redio TBC FM kijulikanacho kwa jina la *Papaso.*

kuwa ili wasanii wa BF waendelee kuwa wachangiaji wazuri wa sanaa hii hawana budi kuishi katika hali ya uduara. Kupitia uduara huo wasanii wa BF huibuka na hung'ara, kisha hupotea, au huibuka, hung'ara kisha huendelea kustawi; na pengine huibuka, na kupotea bila hata kupitia hatua ya kustawi. Kwa hiyo, uhai wa wasanii wa BF umefumbatwa na mzunguko wa duara la kuibuka, kung'ara na kupotea.

## 1.0 Utangulizi

Maana ya muziki wa Bongo Fleva pamoja na aina ya nyimbo zinazounda muziki huo vimekuwa na mjadala mkubwa miongoni mwa wataalamu wanaojadili muziki huo. Masonga (2005) anabainisha kwamba Bongo Fleva inajumuisha miziki hii: muziki wa Kufokafoka/Hip hop, muziki wa Taratibu yaani R&B, Zuku (Zouk), Charanga, muziki wa Kihindi, Chacha, Rumba, Raga, Ngoma za Asili, Taarab, na nyimbo za Kikongo (boringo). Omari (2009) naye anataja aina hizi: muziki wa Kufokafoka, muziki wa Taratibu (*Rhythm and Blues*), muziki wa Haraka (dance hall & raga) na Zuku. Mwanjoka (2011) anatoa aina zifuatazo: nyimbo za Taratibu (R&B), Zuku (zouk), Rege (reggae), Raga, Hip hop, Rumba, Salsa, na aina zingine zinazoakisi maudhui ya Kitanzania na Kiafrika kwa ujumla. Vilevile, Mnenuka (2011) amependekeza uainishaji anaouita wa mpito wa muziki wa Bongo Fleva unaozingatia uchezaji, melodi na midundo ya muziki kama ifuatavyo: Kufokafoka (nyimbo za awali kabisa zijulikanazo kama Rap), Tongozi (nyimbo zinazohusu utongoaji wa mashairi kama za Mrisho Mpoto), Mchazika (mchanganyiko wa Bongo Fleva na aina za nyimbo nyingine zipigwazo hapa Tanzania kama Dansi, Taarab, Mduara na aina zingine kadiri zitakavyoendelea kujitokeza), Mchangageni (mchanganyiko wa melodi na ridhimu za kigeni zinazoimbwa na kwa lugha ya Kiswahili, lugha za kigeni, mchanganyiko wa lugha, au lugha ya jamii mojawapo ya Tanzania; mfano Raga, Dance hall, Rege, Charanga, Salsa, Zuku, R&B), Mchangasili (mchanganyiko wa mahadhi ya ngoma za asili za Tanzania kama vile Mnanda, Segere, Lizombi n.k.), Mchangadini (mchanganyiko wa Bongo Fleva na melodi/ridhimu za kidini hasa dini za kigeni kama Kaswida na nyimbo zingine za Kikiristu), na Mchangalela (mchanganyiko holela ambao haubainishi waziwazi asili yake).

Kwa mujibu wa makala haya, muziki wa Bongo Fleva ni kapu linalojumuisha kila aina ya muziki unaopatikana nchini Tanzania. Msingi wa makala haya kuamini hivyo ni kutokana na sababu kwamba kirai "bongo fleva" kinatokana na maneno mawili: "bongo" lenye maana ya Dar es Salaam ambayo inaiwakilisha Tanzania. Kwa hivyo, Bongo ni sawa na Tanzania. Neno lingine ni "fleva" ambalo linatokana na neno la Kiingereza "flavour" lenye maana ya ladha. Hivyo, "bongo fleva" ni ladha za kimuziki zipatikanazo Bongo/Tanzania.

Muziki wa Bongo Fleva una kategoria mbalimbali kama ilivyooneshwa na wataaalamu mbalimbali hapo awali kama vile Taarab, Zuku, Hip hop, R&B, Rege, Injili, Singeli na Nyimbo za Asili. Makala haya yanamakinikia baadhi ya kategoria tu kama sampuli itayowakilisha kategoria nyingine. Kategoria hizo ni R&B, Zuku, Hip hop na Injili kama ilivyobainishwa katika Jedwali Na. 1 hapa chini:

**Jedwali Na. 1: Kategoria za Muziki wa BF Zilizochunguzwa**

| **Na.** | **Kategoria ya Bongo Fleva** | **Mifano ya Wasanii** |
|---|---|---|
| 1. | R & B, Zuku | Diamond, Alikiba, Jux, PNC, Lady Jay Dee, 20%, Z-Anto, Mr Nice |
| 2. | Hip hop | Roma, Nay wa Mitego, Kalla Pina, Profesa Jay, Kala Jeremiah |
| 3. | Injili | Bahati Bukuku, Rose Mhando, Bonny Mwaitege, Gudlucky Gozbert |

**Chanzo:** Mwandishi (2018)

Licha kuzingatia kategoria zilizotajwa hapo juu, mwandishi wa makala haya anatambua aina kuu tatu za wasanii kwa kuzingatia kigezo cha kuibuka na kung'ara kwao. Ni kawaida kwa kila sekta au tasnia kuendelea kuibuka kwa watu wapya mbalimbali ambao wengine hufanya kazi vizuri na kuacha historia nzuri nchini lakini wengine hufanya mambo mabaya katika nafasi zao na kuacha historia vilevile ingawa ni mbaya. Halikadhalika, hali hiyo imekuwa ikitamalaki katika tasnia ya muziki wa Bongo Fleva. Kwa kuzingatia muktadha huu, wasanii wanaojihusisha na sanaa ya muziki wa Bongo Fleva wapo katika makundi matatu.

Kundi la kwanza hujumuisha wasanii wanaoibuka mara moja na kushindwa kuvuma hatimaye kutopata nafasi ya kusikika kwa watu wengi. Wasanii hao hawapati kufahamika kwa sababu hawajawahi kusikika sana katika vituo vya redio au televisheni. Sababu za wao kutosikika sana ni: kutojipanga vizuri, kutoa nyimbo kwa majaribio tu, kukosa usimamizi (menejimenti) wa miziki yao, na kutokuwa na vipaji vya kuimba (kutoa nyimbo mbaya au zisizovutia).

Kundi la pili ni la wasanii wanaoibuka na kung'ara kwa kawaida. Hawa ni wale wasanii wanaoibuka na kufanya vizuri katika muziki lakini hubakia kuwa kiwango cha kati, yaani hawako kileleni wala hawako chini sana. Mifano ya wasanii kama hawa ni Ditto, Jux, Belle 9, Madee, Christina Shusho, Kala Jeremiah, Bill Nass, na Barnaba.

Kundi la tatu ni la wasanii wanaofanikiwa "kuwika" katika muziki wa Bongo Fleva kwa msingi wa kufanikiwa kuwa juu ya kilele cha muziki. Mifano ya wasanii hawa ni kama vile Rose Mhando, Bahati Bukuku, Bonny Mwaitege, Alikiba, Diamond Platnumz, Dudu Baya, Mad Ice, Bwana Misosi, Ommy Dimpoz, Marlaw, Afande Selle, Q-Chillah/Chief, Ben Pol, Soggy Doggy, Biz Man, Fid Q, Nay wa Mitego, Noorah, Mh. Temba, Ray C, Chegge, Banana Zorro, Roma Mkatoliki, Stamina, Tunda Man, Mr. Nice, Mb Doggy, Z- Anto, AY, Dully Sykes, 20%, Aslay, TID, Mwana FA, Prof Jay, Lady Jay Dee, Juma Nature, Matonya, Mr. 11/Sugu n.k. Hawa ni mifano ya wasanii waliowahi kuwa juu au wako juu daima. Kundi hili la wasanii waliofanikiwa kuwa juu limegawanyika katika sehemu tano:

i. Wasanii waliowahi kuwa juu kisha wakapotea na baadaye wakarudi tena na kuendelea kuwa juu;
ii. Wasanii waliowahi kuwa juu kisha wakapotea katika muziki na baadaye wakarudi kuwa wasanii wa kawaida. Hawakurudi kuwa kileleni kama mwanzo;
iii. Wasanii waliowahi kung'ara katika muziki kisha wakashuka na kuwa wasanii wa kawaida. Hawa hawakuwahi kupotea bali wameshuka kutoka kileleni na kuwa wasanii wa kawaida;
iv. Wasanii waliowahi kuwa juu kisha wakapotea moja kwa moja katika muziki bila kurudi tena katika tasnia ya muziki;
v. Wasanii ambao wamebaki katika kilele pasi kushuka wala kupotea. Jedwali Na. 2 linaonesha mifano ya wasanii katika makundi hayo.

**Jedwali Na. 2: Mgawanyiko[3] wa Wasanii Waliofanikiwa Kung'ara katika Bongo Fleva**

| Kundi la Wasanii | | Mifano ya Wasanii |
|---|---|---|
| 1. | Waliong'ara kisha wakapotea na kurudi tena kung'ara | Ali Kiba |
| 2. | Waliong'ara kisha wakapotea halafu wakarudi na kuwa wasanii wa kawaida | Matonya, Mr 11/Sugu, Dully Sykes, TID, Rose Mhando, Bonny Mwaitege, Dudu Baya, Q-Chillah/ Chief |
| 3. | Waliong'ara kisha wakashuka na kuwa wasanii wa kawaida | Lady Jay Dee, Prof Jay, AY, Mwana FA, Ommy Dimpoz, Bahati Bukuku, Tunda Man, Mh. Temba, Chegge, Fid Q |
| 4. | Waliong'ara kisha wakapotea moja kwa moja | Juma Nature, Mb Doggy, Mr Nice, Z – Anto, 20%, Biz Man, Soggy Doggy, Noorah, Ray C, Banana Zorro, Marlaw, Mad Ice, Bwana Misosi |
| 5. | Waliong'ara/wanaong'ara pasi kupotea/kushuka | Diamond, Aslay, Nay wa Mitego, Roma Mkatoliki, Stamina, Ben Pol |

**Chanzo:** Mwandishi (2018)

Kategoria za muziki wa Bongo Fleva zinazomakinikiwa na makala haya (Zuku, R & B, Hip-hop, na Injili/Dini) zina hadhi tofautitofauti. Muziki wa Injili unaonekana kupata mtazamo chanya kutoka kwa jamii. Mwandishi wa makala haya ambaye pia anajihusisha kwa namna fulani na muziki wa Bongo Fleva hususani katika kategoria ya kwanza (Zuku, R&B) amewahi kupokea ushauri kutoka kwa marafiki na mashabiki wake kwamba afanye muziki wa Injili. Ijapokuwa watoa ushauri hao hawakuweka bayana na kwa namna ya moja kwa moja sababu za kushauri hivyo, mwandishi alibaini kwamba wao (marafiki na mashabiki) wana mtazamo

3 Hii ni kulingana na hali ya wakati ambapo makala haya yanaandikwa/yanachapishwa. Inawezekana hali isiwe hivyo baada ya muda fulani kupita.

hasi kwa kategoria kadhaa za Bongo Fleva kama vile Zuku, R&B, Hip hop, rege na Singeli. Sababu zinazowafanya baadhi ya watu wawe na mtazamo hasi kwa kategoria hizo za Bongo Fleva ni kutokana na sababu kwamba baadhi ya nyimbo katika kategoria tajwa hazina maadili ya Kitanzania, hivyo, zinaonekana kuwa ni nyimbo za kihuni (zilizokosa ustaarabu na staha). Madai haya yanapingwa na baadhi ya wataalamu akiwamo Samwel (2010/2011) na kuwataka watu wabadili mtazamo huo finyu na hasi kwa sababu si wasanii wote wanaimba nyimbo zisizo na maadili.

Makala haya yanaunga mkono mawazo ya Samwel kwa sababu wapo wasanii katika kategoria hizo wanafanya muziki unaofuata maadili ya Kitanzania kama vile Alikiba, Ommy Dimpoz, 20%, Profeza Jay, n.k. Saula la watu wachache kukengeuka katika tasnia fulani lipo katika kila sekta, kwa hivyo, siyo sawa kufanya majumuisho kwa kutumia sampuli ndogo. Kila siku tunashuhudia vyombo vikiripoti watu mbalimbali wakiwamo viongozi wa sekta mbalimbali kwenda kinyume na maadili ya kazi zao; lakini sekta hizo hazijawahi kuitwa sekta za kihuni.

## 2.0 Kuibuka na Kung'ara kwa Wasanii wa Bongo Fleva

Makala haya yamebaini kuwa kuna sababu tatu za msingi zinazowafanya wasanii kuibuka na kung'ara katika muziki wa BF. Baadhi ya sababu hizo ni kama vile kuwa na kipaji kizuri cha kuimba, kujituma, udhamini au menejimenti nzuri.

Kutokana na utafiti uliofanywa na mwandishi wa makala haya imebainika kuwa sauti nzuri na uwezo wa kutunga mashairi yenye mvuto na yanayopendwa ni jambo la kwanza linalomfanya msanii kusikilizwa na kupendwa na wengi. Wimbo wowote mzuri wenye melodi na mashairi mazuri ukishasikilizwa na watu, lazima upendwe. Elimu ya sanaa pia ina nafasi yake katika muziki; lakini haijwekwa kama kategoria inayojitemea kwa sababu nchini Tanzania, wasanii wengi waliofanikiwa katika muziki hawajasomea sanaa/muziki bali wanatumia vipaji vyao tu.

Jambo la pili lililochangia hali hii ni kujituma. Kujituma ni hali ya kufanya kazi kwa juhudi kubwa. Hii inahusisha kuvumilia shida mbalimbali ambazo mmoja anakumbana nazo katika mchakato wa muziki, kutokata tamaa na kutovunjika moyo pale anapokumbana na magumu. Suala la kujituma na kuwa mvumilivu ni moja ya siri za mafaniko katika kila tasnia. Kwa hivyo, wasanii wote wenye uvumilivu na hali ya kujituma hufanikiwa sana katika muziki wao.

Kadhalika, mwandishi amegundua kuwa jambo lingine lililochangia kuinuka na kustawi kwa baadhi ya wasanii ni udhamini na menejimenti nzuri. Udhamni ni kitendo cha baadhi ya watu wenye uwezo na nia ya kuwekeza katika muziki, kuamua kuwasimamia wasanii wa muziki wa BF. Usimamizi huo unahusisha kutoa pesa kwa ajili ya msanii kurekodi nyimbo, kusimamia nyimbo hizo ziweze kupigwa katika vituo mbalimbali vya redio na televisheni, kumtafutia msanii nafasi ya kufanya matamasha, na kutafuta soko la muziki wa msanii. Mfano wa Mameneja waliowahi kuwasimamia au wanaowasimamia wasanii ni Abdu Bonge aliyewahi kuwa Meneja wa kundi la Tip-Top Connection, Ustadhi Juma Namusoma aliwahi kuwa Meneja wa msanii PNC, Said Fella aliwahi kuwa Meneja wa TMK Wanaume Family, na Ya Moto Band. Vilevile, Saidi Fella, Sallam, na Babu Tale wanashirikiana kumsimamia Diamond Platnumz na kundi zima la Wasafi Classic Baby (WCB).

Mafanikio ya kimuziki ya Diamond Platinumz mwenye mameneja watatu ni makubwa sana. Kwa hiyo, inawezekana kabisa kwamba mafaniko hayo yanachangiwa na kuwapo kwa mameneja hao. Kwa hivyo, endapo msanii atapata meneja mzuri na makini atakuwa na menejimenti nzuri ya muziki wake; hatimaye, kung'ara katika muziki.

## 3.0 Kushuka au Kupotea kwa Wasanii wa Bongo Fleva

Miongoni mwa wasanii waliowahi kung'ara kisha wakapotea ni Mr. Nice (aliyeng'ara miaka ya 2001-2007), Z-Anto (aliyeng'ara 2005-2010) na 20% (aliyeng'ara 2005-2012), Bonny Mwaitege & Rose Mhando (2005-2015) na Afande Selle (aliyeng'ara 2001-2012). Sababu za wasanii wa Bongo Fleva hususani katika kategoria ambazo makala haya yamezimakinikia ziko katika makundi manne: sababu za kiuelewa (kuelewa mambo mbalimbali), sababu za kiutandawazi na usasa, sababu za kielimu (elimu ya darasani), sababu za kimenejimenti, migogoro baina ya wasanii, kuingia katika mgogoro na BASATA. Sababu hizi zinafafanuliwa mojamoja lakini kwa namna ambayo haitatolewa mifano ya wasanii katika kila sababu. Imefanywa hivyo kwa sababu za kiitikeli. Hii inatokana na sababu kwamba hakuna binadamu ambaye anapenda kuumizwa au kudhalilishwa hata kama jambo hilo ni la kweli. Kung'ara na kupotea kwa wasanii hao kumechangiwa na sababu mbalimbali kama ilivyojadiliwa hapa chini:

**a) Sababu za Kiuelewa (uelewa wa masuala mbalimbali)**

Hii ni sababu inayohusu wasanii kutokuwa na uelewa mkubwa wa masuala ya muziki hapa nchini. Wasanii wengi siyo tu kwamba hawana elimu ya sanaa/muziki, hawana hata elimu ya sekondari na/au chuo kikuu. Ni dhahiri kwamba elimu ya darasani ina nafasi yake kubwa tu katika maisha. Elimu hiyo haiwezi kubezwa hata kidogo na mtu akiikosa. ni dhahiri anapungukiwa na maarifa ya kuendesha maisha yake. Kwa hivyo, kukosekana kwa elimu hiyo kunaweza kuchangia msanii kutojua mwenendo mzima wa sanaa anayoifanya. Kutojua mwenendo wa muziki ni tatizo kubwa kwa sababu linapojitokeza tatizo, mathalani la kushuka katika ngazi ya kimuziki aliyopo, ni ngumu kujua kilichosababisha ashuke na hatimaye kutojua afanyeje ili aweze kurudi katika ngazi hiyo. Baadhi ya wasanii hao walioshuka na kupotea katika muziki walijikuta wako kileleni ilhali hawajui ni kwa nini wako katika kilele cha muziki. Vivyo hivyo, walipoanguka, hawajui mpaka leo ni nini kimesababisha waanguke. Hili linaenda sambamba na msanii kutotambua kwamba anapofikia ngazi fulani ya juu kimafanikio hatakiwi tena kujiendesha mwenyewe peke yake bali inabidi ajiendeshe kama kampuni. Hii inamaanisha kuwa anatakiwa awe na kampuni yenye uongozi madhubuti. Jambo hili la kutambua ngazi kubwa ya kimafanikio iliyofikiwa na kufanya hili linaloelezwa hapa, limeweza kutekelezwa ipasavyo na msanii Diamond Platnumz. Yeye alianza kujiendesha kama msanii peke yake lakini baadaye alipoona amefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika muziki akaamua kujiendesha kama kampuni. Matunda ya kufanya hivyo yanaonekana wazi kwa msanii huyo ambapo ameendelea kuwa kileleni kwa muda mrefu katika muziki wa Bongo Flveva.

**b) Sababu ya Kiutandawazi na Usasa**

Ijapokuwa utandawazi una faida kubwa kama vile nyimbo kuwafikia watu kwa njia nyingi kwa haraka, kujenga ushirikiano wa kimuziki kwa kirahisi na haraka na mataifa mengine n.k., bado utandawazi huo unasababisha wasanii wa Bongo Fleva waanguke pasi kuweza kusimama tena katika muziki wa Bongo Fleva. Baadhi ya wasanii baada ya kuwa kileleni, wanalewa sifa na kujikuta wakiendeshwa na utandawazi badala ya wao kuuendesha utandawzi huo. Wasanii hao wamekuwa wakilazimisha kuishi maisha yanayoendana na utandawazi na usasa sana kiasi cha kuishi maisha ya juu yanayozidi kipato chao. Kwa mfano, wasanii hao hulazimisha

kununua vitu vya gharama kubwa ambavyo havina faida kubwa kwao kama vile simu, gari, kutafuta rafiki wa kimapenzi wa gharama n.k. Wasanii hao wanaamini kufanya baadhi ya mambo (hata kama ni hatarishi na haramu) ndiyo kwenda na usasa na utandawazi. Mambo hayo ni kama kujiingiza katika uvutaji wa bangi, matumizi ya dawa za kulevya, ulevi na umalaya. Mambo hayo pia si mapya kwa wanaofuatilia muziki wa Bongo Fleva. Ni kawaida kuona magazeti yameripoti habari mbalimbali zinazosawiri mambo hayo yaliyobainishwa. Mfano wa taarifa hizo ni kama vile wasanii kuwa na mahusiano ya kipamenzi na watu wengi, wasanii kuonekana wakitumbuiza huku wamelewa, wasanii kufika katika mahojiano ya kipindi katika redio au televisheni huku wakionekana wamelewa, baadhi ya wasanii kukiri wazi kwamba walikuwa wanatumia dawa za kulevya (hatimaye kuwa waathirika wa dawa hizo) na sasa wapo katika kliniki ya tiba ili warudi katika hali yao ya kawaida, n.k. Masuala haya yote husababisha wasanii hao kufirisika na kujikuta hawana hata pesa za kurekodia wimbo pamoja na za kulipia katika vyombo vya habari ili wimbo uweze kupigwa/kutangazwa.

**c) Sababu za Kielimu (elimu ya darasani)**

Ni suala lisilopingika kwamba elimu ya darasani ina nafasi yake katika uendeshaji wa maisha japo inaweza isiwe na mchango wa moja kwa moja katika sanaa ya muziki wa Bongo Fleva. Wasanii wengi wa Bongo Fleva wameishia darasa la saba. Baadhi yao wamebahatika kuishia kidato cha nne na wachache sana wana elimu ya kidato cha sita au/na chuo kikuu. Hali kadhalika, wasanii wengi (zaidi ya 90%) nchini Tanzania hawana Elimu ya muziki au sanaa. Kukosekana kwa elimu hiyo kunachangia wasiwe na maarifa ya ziada ya kuweza kusimama vizuri katika muziki wao.

**d) Sababu za Kimenejimenti**

Menejimenti ni uongozi wenye jukumu la kumsimamia msanii. Wako wasanii ambao kung'ara kwao kulitokana na menejimenti nzuri. Menejimenti ikiyumba inasababisha msanii kushuka katika muziki na hatimaye kupotea. Kuyumba kwa menejimenti kunaweza kusababishwa na msanii mweyewe kutokana na hoja zilizotolewa katika kipengele (b) au sababu nyingine zinazotokana na upungufu wa namna mbalimbali katika menejimenti yenyewe. Aidha, ifafahamike kwamba umekuwa ni utamaduni wa wasanii wa muziki Bongo Fleva kusimamiwa na menejimenti/watu fulani. Kwa mfano, Abdu Bonge alikuwa Meneja wa kundi la

wasanii liitwalo Tip-Top Connection, Ustadhi Juma Namusoma alikuwa Meneja wa msanii PNC. Pia, Babu Tale, Sallam, na Said Fella ni Mameneja wa Diamond Platnumz na kundi lake la WCB. Imeshuhudiwa kupitia mahojiano mbalimbali ya wasanii wakikiri kwamba waliyumba kimuziki baada ya kutofautiana na menejimenti inayowasimamia.

**e) Migogoro Baina ya Wasanii**

Ugomvi baina ya wasani umekuwa sababu mojawapo ya kuwavuruga kimuziki. Yapo baadhi ya makundi ya muziki yaliyosambaratika baada ya wasanii waliokuwa wakiunda makundi hayo kugombana. Mfano wa makundi hayo ni Wanaume TMK waliogawanyika na kuundwa kwa Wanaume Halisi na Wanaume Family; lakini haya makundi mawali yaliyoundwa baada ya mpasuko hayana nguvu kubwa kama lilivyokuwa kundi la mwanzo. Makundi mengine yaliyowahi kufanya vizuri na baadaye yakavunjika kutokana na migogoro baina ya wasanii ni Wakali Kwanza, Top Band, naTip-Top Connection. Popote penye migogoro hapawezi kuwa na maendeleo au mafanikio.

**f) Kuingia Mgogoro na BASATA kwa Kutoa Nyimbo Zisizo na Maadili**

BASATA ni chombo kinachohakikisha sanaa nchini Tanzania inaendeshwa kwa kufuata taratibu, kanuni na maadili ya Kitanzania. Wasanii wanaokiuka kanuni na taratibu hizo ndio wanaoingia katika mgogoro na BASATA, na hatimaye kupewa adhabu. Kuna baadhi ya wasanii waliwahi kuonywa na kupewa adhabu na BASATA kwa kutoa nyimbo zisizo na maadili. Mathalani, Machi 2018, Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) lilizifungia nyimbo 15 kama zilivyobainishwa katika Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3: Nyimbo za Bongo Fleva Zilizofungiwa na BASATA 2018**


| Na. | Jina la Wimbo | Jina la Msanii |
|---|---|---|
| 1. | Hallelujah | Daimond Platnumz |
| 2. | Wakawaka | Nay wa Mitego |
| 3. | Kibamia | Roma na Stamina (Rostam) na Maua Samma |
| 4 | Pale kati Patamu | Nay wa Mitego |
| 5 | Hainaga Ushemeji | Man Fongo |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | *I am Sorry* "Samahani" (Tafsiri yangu) | Nikki Mbishi |
| 7 | Chura | Snura |
| 8 | Tema Mate Tuwachape | Madee |
| 9 | Uzuri Wako | Jux |
| 10 | Nampa papa | Gigy Money |
| 11 | Nampaga | Barnaba Classic |
| 12 | Maku Makuz | Nay wa Mitego |
| 13 | Nimevurugwa | Snura |
| 14 | Bongo Bahati Mbaya | Young Dee |
| 15 | Mikono juu | Nay wa Mitego |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na BASATA

Jedwali Na. 3 linaonesha nyimbo zilizofungiwa na BASATA kwa sababu ya nyimbo hizo kukosa maadili. Mathalani, wimbo wa "Kibamia" wa Rostam wakimshirikisha Maua Samma ulikuwa unatoa tafsiri kuwa mwanamume mwenye maumbile madogo katika sehemu zake za siri hawezi kuwa hodari wa tendo la ndoa. Hili linadhihirishwa na mstari mmojawapo katika wimbo huo usemao: *"Nani atanifaa na kwenye kitanda atanipa raha?, sitaki kibamia, mwanaume mashine…."*. Mstari huu kutoka katika wimbo huo, ni sehemu mojawapo inayoashiria wimbo huo kukosa maadili.

Vilevile, mnano tarehe 18/12/2018, BASATA liliwafungia wasanii Dimond Platnumz na Rayvan kufanya tamasha lolote kwa muda usiojulikana kutokana na kutoa wimbo wao ujulikanao kwa jina la "Mwanza". Picha Na. 1 ni barua ya BASATA kwa wasanii hao.



National Arts Council BASATA

Tarehe: 18/12/2018

BASATA Arts Centre

Tel. 2863748/2860485

Fax: 0255- (022) – 286 0486

Ilala Sharif Shamba

P.O.Box. 4779, Dar es Salaam

E-mail: info@basata.go.tz

**TAARIFA KWA UMMA**

Baraza la Sanaa la Taifa **(BASATA)** limewafungia wasanii wa muziki wa kizazi kipya **Nasib Abdul** (***Diamond Platnumz***) na **Raymond Shaban Mwakyusa (Rayvan)** kutofanya onyesho lolote ndani na nje ya nchi kwa muda usiojulikana kuanzia leo tarehe 18/12/2018.

Itakumbukwa kuwa mnamo tarehe 12/11/2018, BASATA ilitoa taarifa kwa Umma kuhusu kufungia wimbo unaojulikana kwa jina la **"Mwanza"**.

Baraza limefikia maamuzi ya kuwafungia rasmi kutokana na Wasanii hawa kuendelea kuonyesha dharau na utovu wa nidhamu kwa Mamlaka zinazosimamia Masuala ya Sanaa nchini na uvunjifu wa maadili uliokithiri unaofanywa na waandaaji wa Tamasha la Wasafi 2018 chini ya uongozi wake **Nasib Abdul** (***Diamond Platnumz***).

Pamoja na maelezo hayo, Baraza linatoa taarifa kuwa kibali cha Tamasha la Wasafi 2018 kimesitishwa kutokana na ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na taratibu katika uendeshaji wa tamasha hilo hapa nchini.

**"Sanaa ni kazi, tuipende, tuikuze na kuithamini"**

**Onesmo Kayanda**

**Kny: KATIBU MTENDAJI**

*Barua zote ziandikwe kwa Katibu Mtendaji*

All correspondence to be addressed to The Executive Secretary

*Picha Na. 1: Barua ya BASATA ya Kuwafungia Wasanii Kufanya Matamasha*


Miongoni mwa mambo yaliyosababisha wimbo huo kuonekana kukosa maadili ni pale wanapotaja kwa kifupi kata iliyopo mkoani Mwanza iitwayo Nyegezi. Wasanii hao walikuwa wamefupisha jina hilo katika wimbo huo kwa kuiita kata hiyo "nyege" kama ilivyonukuliwa katika moja ya mistari katika wimbo huo: "*eh nyege nyege, kwetu Mwanza Nyegezi, eh nyege nyege, kwetu Mwanza Nyegezi*". Kwa hivyo, kutokana na neno "nyege' kuwa na maana nyingine, ilisababisha baadhi ya watu pamoja na BASATA waone kwamba wasanii hao wamelifupisha neno hilo kwa makusudi huku wakiwa na maana ya msingi ya neno hilo na si kifupisho cha kata ya Nyegezi.

## 4.0 Uduara katika Mwenendo wa Wasanii wa BF

Mwenendo wa wasanii wa Bongo Fleva nchini Tanzania ukitazamwa kwa jicho la kiuchambuzi/kiuchunguzi, utaona kwamba wanajikita katika mzunguko wa namna fulani mithili ya umbo la duara. Kwa kiasi kikubwa mzunguko huo ndio njia wanayopita wasanii wengi katika kujihusisha na tasnia ya nyimbo za BF. Uduara huo hujitokeza pale msanii anapoibuka na kung'ara halafu baadaye anapotea kisha anarudi tena katika muziki kama ionekanavyo katika Mchoro Na. 1.

Mfano wa wasanii walioiishi nadharia-tete hii ya uduara ni Alikiba ambaye miaka ya 2005-2010 aliwika na kung'ara sana katika muziki wa Bongo Fleva. Miaka ya 2012-2016 akapotea katika muziki kisha akaja kuibuka tena 2017. Mwingine ni Dully Sykes aliyewahi kuwa kileleni katika muziki huo miaka ya 2000-2010. Baada ya hapo akawa amepoa kimuziki na akaja kuibuka tena kwa kasi kubwa mwaka 2017, upo uwezekano kuwa kuna siku atang'ara tena.

Wapo wasanii ambao wametajwa katika makala haya kama wasanii ambao kwa sasa wamepotea katika muziki. Swali laweza kuwa, je, hawa wanaingiaje katika nadharia-tete hii ya uduara. Jibu ni kwamba kwa kuwa wasanii hao bado wapo hai, mtazamo wa nadharia-tete hii ni kwamba kuna muda wataibuka tena katika muziki na kung'ara, hivyo, kukamilisha hali ya uduara.




*Mchoro Na. 1: Uduara katika Muziki wa Bongo Fleva*

**Chanzo:** Mwandishi (2018)

Kwa hivyo, mchoro huu unaonesha kwamba msanii wa BF huibuka, hung'ara kwa wakati fulani kisha hupotea; na baada ya muda huibuka tena na kujikuta akizunguka katika duara hilo. Ifahamike kwamba nadharia yoyote lazima iwe na vighairi. Kwa hivyo, si lazima wasanii wote waingie katika uduara huu. Aidha, wapo wasanii watakaoingia katika nadhariatete hiyo kwa kiasi fulani, kwa maana kwamba wanaweza wasikamilishe duara lote.

## 6.0 Hitimisho

Nadharia-tete iliyoibuliwa na makala haya hailengi kuwaelekeza wasanii waifuate kwa msingi kwamba wahakikishe kuwa wanaibuka, wanang'ara na baadaye wafanye mikakati ya makusudi ya kupotea kisha kuibuka tena; la hasha, bali nadhariatete hiyo imeibuliwa kwa kuzingatia kinachotokea katika muziki huo wa BF. Hivyo, nadhariatete hii ni msingi wa uelezaji kimapana wa hali hiyo ya muziki (uduara) nchini Tanzania. Kwa msingi huo basi, wasanii wa muziki wa Bongo Fleva wanatakiwa kutambua kuwa muziki huo ni ajira kubwa sana katika maisha yao na kupata nafasi ya kusikika katika jamii ndani na nje ya Tanzania (kuwa na mashabiki wengi) ni mtaji mkubwa. Kwa hivyo, hawatakiwi kuichezea bahati hiyo kwa kufanya makosa yanayosababisha wazorote katika muziki wao. Wasanii wanatakiwa kujifunza kutokana na wenzao waliowahi kung'ara katika muziki na kisha kupotea pasi kuwa na uwezo wa kurudi tena kileleni haraka. Aidha, wasanii

wanaoibukia sasa wanatakiwa kujifunza kwa wasanii kama Diamond, Aslay, Nay wa Mitego, Roma Mkatoliki, Stamina, na Ben Pol na ambao wameonekana kudumu katika kilele cha muziki kwa muda mrefu kama ilivyoelezwa katika kipengele cha 3.0. Jambo la msingi ambalo msanii anatakiwa kulifahamu ni kuuelewa muziki wa Bongo Fleva hususani kategoria aliyopo. Yawezekana masuala mengine hayako wazi katika muziki huo lakini wasanii wanatakiwa kuyajua na kuyafuata pamoja na kushika miiko yake ipasavyo.

**Marejeleo**

Omari, S (2009). Tanzania Hip Hop as Popural Literature. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mahenge, E. (2010/2011). Chimbuko la Muziki wa Hip Hop ni Uasi au Sanaa za Maonesho? *Mulika*: Toleo Maalum la Muziki wa Kizazi Kipya. Juz. 29/30. Kur. 3-15.

Mangesho, P. (2003). Global Cultural Trends: The Case of Hi hop Music in Dar es Salaam.Tasnifu ya Umahairi (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mnenuka, A. (2010/2011). Taswira ya Mwanamke katika Muziki wa Bongo Fleva: Mifano kutoka katika Nyimbo Teule. *Mulika*: Toleo Maalum la Muziki wa Kizazi Kipya. Juz. 29/30. Kur. 69-87.

Mwanjoka, G. (2011). Harakati za Bongo Fleva na Mapinduzi. Dar es Salaam: Hakuna Mchapaji/mchapishaji.

Perullo, A. (2007). 'Here's a Little Something Local': An Early History of Hip Hop in Dar es Salaam, Tanzania, 1984-1997. Dar es Salaam: The History of an Emerging East African Metropolis. *British Institute and Mkuki na Nyota*. uk. 250-272.

Samwel, M. (2010/2011). Masuala ya Kisiasa katika Mashairi ya Kimapenzi ya Muziki wa Bongo Fleva. *Mulika*: Toleo Maalum la Muziki wa Kizazi Kipya. Juz. 29/30. Kur. 16-27.